



JARIDA LA MTANDAONI
TOLEO NAMBA 174 | JULAI 04, 2022

UGENI KUTOKA NCHINI ZIMBABWE WAFURAHISHWA NA UZALISHAJI WA SUMAJKT



Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT Kanali Shija Lupi (kushoto) akifafanua Jambo katika kikao na Ugeni kutoka Zimbabwe, Kulia ni Mkunzi Mkuu wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu nchini Zimbabwe Kanali Cosmas Kahondera.

UGENI KUTOKA NCHINI ZIMBABWE WAFURAHISHWA NA UZALISHAJI WA SUMAJKT

Mkunuzi Mkuu kutoka Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC) nchini Zimbabwe, Kanali Cosmas Kahondera, amesema kuwa wamejifunza na kufurahishwa na Uzalishaji wa bidhaa mbalimbali unaofanywa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT).

Kanali Kahondera, amezungumza hayo leo tarehe 04 Julai 2022, alipofanya ziara ya kimafunzo katika kiwanda cha Maji (SUMAJKT BOTTLING CO. LTD) na Nguo (SUMAJKT GARMENT CO. LTD) akiwa pamoja na wakufunzi na wanafunzi wa chuo hicho idadi 28 Mgulani JKT jijini Dar es salaam.

Aidha, Kanali Kahondera, ameongeza kuwa katika Jeshi la Ulinzi nchini Zimbabwe wanayo Taasisi ya Uzalishaji lakini haizalishi bidhaa nyingi kama SUMAJKT.

"Taasisi ya Uzalishaji Mali ya Jeshi letu la Ulinzi Zimbabwe inafanyakazi za uchimbaji wa madini, Usambazaji wa Umeme na Ujenzi wa Majengo" alisema Kanali Kahondera.

Nae Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT Kanali Shija Lupi, ameupokea ugeni huo kwa niaba ya

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa na Afisa Mtendaji Mkuu wa SUMAJKT Meja Jenerali Rajabu Mabele.

Kanali Lupi, amebainisha kuwa ugeni huo umeonesha kufurahishwa na Uzalishaji wa maji ya kunywa ya Uhuru Peak pamoja na Ushonaji wa Nguo mbalimbili unaofanywa na SUMAJKT.

Aidha, Kanali Lupi ameeleza kuwa ugeni huo umesema ukipata fursa nyingine utakuja kutembelea SUMAJKT.

Ameongeza kuwa, katika historia Tanzania na Zimbabwe ni nchi zenyé mahusiano mazuri toka enzi za wapigania Uhuru.

Ziara ya wanafunzi kutoka chuo cha Ukamanda na Unadhimu nchini Zimbabwe wametoka katika nchi nne tofauti ambazo ni Afrika Kusini, Lesotho, Tanzania na Zimbabwe.

SUMAJKT imekuwa ikipokea ziara mbalimbali za kimafunzo kutoka nchi tofauti kwa ajili ya kujifunza shughuli za Uzalishaji Mali.

Matukio Katika Picha

Mkufunzi Mkuu kutoka Chuo cha Ukamanda na Unadhimu nchini Zimbabwe Kanali Cosmas Kahondera, akisaini kitabu cha wageni alipowasili Kikosi cha Mgulani JKT jijini Dar es Salaam.



Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji SUMAJKT Kanali Shija Lupi akizungumza na Wakufunzi na Wanafunzi kutoka Chuo cha Ukamanda na Unadhimu nchini Zimbabwe (hawapo pichani).

Baadhi ya Wakurugenzi na Wakuu wa Miradi SUMAJKT wakifuatilia kikao cha ziara ya Wakufunzi na Wanafunzi kutoka Chuo cha Ukamanda na Unadhimu nchini Zimbabwe kilichofanyiwa katika ukumbi wa Isamhuyo Mgulani JKT jijini Dar es salaam.



Matukio Katika Picha

Baadhi ya Wakufunzi na wanafunzi kutoka Chuo cha Ukamanda na Unadhimu nchini Zimbabwe wakiwa katika kikao na SUMAJKT kwenye ukumbi wa Isamuhyo Mgulani JKT jijini Dar es Salaam.



Mkufunzi Mkuu kutoka Chuo cha Ukamanda na Unadhimu nchini Zimbabwe Kanali Cosmas Kahondera (kulia) akioneshwa baadhi ya nguo zinazoshonwa na kiwanda cha SUMAJKT Garment Company Ltd na Mkurugenzi Mwendeshaji wa kiwanda hicho Meja Sylvester Ntandu.

Mkufunzi Mkuu wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC) nchini Zimbabwe Kanali Cosmas Kahondera (kulia) akioneshwa baadhi ya nguo zinazoshonwa na kiwanda cha SUMAJKT Garment Company Ltd na Mkurugenzi Mwendeshaji wa kiwanda hicho Meja Sylvester Ntandu.



Matukio Katika Picha

Mkufunzi Mkuu kutoka Chuo cha Ukamanda na Unadhimu nchini Zimbabwe Kanali Cosmas Kahondera (katikati) Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT Kanali Shija Lupi (watatu kutoka kushoto) Mkurugenzi Mwendeshaji SUMAJKT Guard Ltd Kanali Joseph Masanja (wakwaza kushoto), Kamanda Kikosi cha Mgulani JKT Luteni Kanali Sylvester Sambila (wapili kulia), wakiwa katika picha ya pamoja na Wakufunzi na Wanafunzi wa Chuo hicho Mgulani JKT.



Mkufunzi Mkuu kutoka Chuo cha Ukamanda na Unadhimu nchini Zimbabwe Kanali Cosmas Kahondera (katikati) Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT Kanali Shija Lupi (watatu kutoka kushoto), Mkurugenzi Mwendeshaji SUMAJKT Guard Ltd Kanali Joseph Masanja (wa kwanza kushoto), Kamanda Kikosi cha Mgulani JKT Luteni Kanali Sylvester Sambila (wa pili kulia), wakiwa katika picha ya pamoja Waku-rugenzi waendeshaji wa Kampuni na Wakuu wa Miradi SUMAJKT katika Kikosi cha Mgulani JKT jijini Dar es Salaam.

Mkufunzi Mkuu kutoka Chuo cha Ukamanda na Unadhimu nchini Zimbabwe Kanali Cosmas Kahondera (katikati), Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT Kanali Shija Lupi (watatu kutoka kushoto), Mkurugenzi Mwendeshaji SUMAJKT Guard Ltd Kanali Joseph Masanja (wakwaza kushoto), Kamanda Kikosi cha Mgulani JKT Luteni Kanali Sylvester Sambila (wapili kulia), wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Waku-rugenzi wa SUMAJKT katika Kikosi cha Mgulani JKT jijini Dar es salaam.

